



## TANGAZO

### UUZAJI WA MAZAO YA MISITU YALIYOPO KATIKA KITUO MENEJA WA MISITU WILAYA YA TANGA

1. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) unatarajia kuuza mazao ya misitu (Slipa) **1740** zenye ujazo wa CBM **249.92398** kwa njia ya mnada zilizopo katika Ofisi ya Meneja Misitu Wilaya ya Tanga tarehe **28.04.2020 saa 04:30 asubuhi**. Mazao (Slipa) yote yatauzwa kama yanavyoonekana katika eneo husika na Mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo. Uzaji huu utafanyika kwa kuzingatia kanuni 31 (ii) ya kanuni za sheria ya misitu za mwaka 2004.
2. Mnada utaendeshwa hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika eneo yalipohifadhiwa mazao.
3. Mshiriki atatakiwa kuwasilisha leseni ya biashara, Usajili wa biashara ya mazao ya misitu husika (2019/2020) na cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN).
4. Wanunuzi wanakaribishwa kutembelea na kukagua mazao hayo wakati wa saa za kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:30) alasiri isipokuwa siku za sikukuu. Wasiliana na Meneja wa Misitu Wilaya (District Forest Manager "DFM") au msaidizi wake kwa msaada wa kutembelea na kukagua mazao hayo.
5. Mnunuzi atakayeshinda atalipa asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani yote ya ununuzi ndani ya siku tatu (3) baada ya kushinda.

Fedha hizo hazitarudishwa. Asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne baada ya mnada. Malipo ya CESS kwa H/W yamo ndani. Malipo yote yatafanyika kwenye akaunti za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) zilizopo kwenye benki ya **NMB, NBC, CRDB na Benki ya Posta** kupitia Mfumo wa **GePG** (Government electronic Payment Gateway) baada ya kupewa Hati ya Madai kutoka kwa DF wa wilaya husika. Kadhalika, Hati ya Madai imeonesha **mitandao ya simu** inayoweza kutumika kulipia maduhuli ya serikali.

6. Mnunuzi atapaswa kuwasilisha hati ya malipo kwa DFM kama uthibitisho wa malipo si zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika
7. Mteja atatakiwa kuondoa mazao ya misitu aliyonunua ndani ya siku 14 tangu tarehe ya kufanyika kwa mnada.
8. Tangazo hili pia linapatikana katika tovoti zifuatazo za Wakala na Wizara: [www.tfs.go.tz](http://www.tfs.go.tz), na [www.mnrt.go.tz](http://www.mnrt.go.tz).

## **ANGALIZO**

**Mshiriki atakayeshinda na kupewa hati ya ushindi na kisha yeye mwenyewe kushindwa kulipia mgawo huo ndani ya muda aliopewa (kadiri inavyoelezwa katika kipengele 11 cha tangazo hili) kwa sababu yoyote ile, atakuwa ametenda kosa la kuhujumu mnada na kwa makusudi kuikosesha Serikali mapato hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kudaiwa fidia ya hasara itakayosababishwa na kitendo hicho chini ya Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi (Sura ya 200 marejeo ya 2002).**

Limetolewa na  
**KAMISHNA WA UHIFADHI**  
**WAKALAWA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA**  
**S.L.P 40832**  
**DAR ESSALAAM**  
**13.04.2020**